**HOTUBA YA MHE. ANTHONY PETER MAVUNDE (MB.), WAZIRI WA MADINI KATIKA HAFLA YA KUFUNGA MKUTANO WA KIMATAIFA WA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA YA MADINI TANZANIA 2023**

***Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Waheshimiwa Mawaziri mliopo;***

***Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini;***

***Waheshimiwa Naibu Mawaziri mliopo;***

***Mheshimiwa Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;***

***Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya mliopo;***

***Komredi Abbas Mtemvu, Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Dar es Salaam;***

***Viongozi wote wa Vyama vya Siasa mliopo;***

***Mheshimiwa Mathayo David Mathayo (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Wajumbe wote wa Kamati ulioambatana nao;***

***Waheshimiwa Wabunge mliopo;***

***Ndugu Kheri Mahimbali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini;***

***Makatibu na Naibu Makatibu Wakuu mliopo;***

***Waheshimiwa Mabalozi mnaowakilisha nchi zenu;***

***Viongozi wa Dini mliopo;***

***Viongozi wote wa Serikali na Taasisi mbalimbali mliopo;***

***Wadau wote wa Sekta ya Madini mliopo;***

***Ndugu Waandishi wa Habari;***

***Mabibi na Mabwana;***

***"Jamhuri ya Muungano wa Tanzania"***

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kujumuika pamoja katika hafla hii ya kilele cha Mkutano huu wa Kimataifa wa Madini na Uwekezaji Tanzania. Nitumie nafasi hii ya kipekee kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali mwaliko wa kushiriki na kuwa Mgeni Rasmi katika kuhitimisha Mkutano huu. Aidha, napenda kuwashukuru washiriki wote kutoka ndani na nje ya nchi kwa kushiriki Mkutano huu kikamilifu. Ushiriki wa kila mmoja umefanya mkutano huu uwe na mafanikio makubwa. Pia, niwashukuru wote walioshiriki kwa namna moja ama nyingine kuwezesha mkutano huu kufanyika kwa ufanisi hadi leo tunapofikia kilele cha mkutano.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Mkutano huu ni muhimu sana kwa Sekta ya Madini kutokana na kwamba unakutanisha wadau muhimu wanaojihusisha na shughuli mbalimbali katika mnyororo mzima wa thamani wa madini. Aidha, Mkutano huu unatoa nafasi kwa wadau wa Sekta ya Madini kubadilishana ujuzi na uzoefu katika masuala mbalimbali yanayohusu shughuli za madini pamoja na kutoa maoni na mapendekezo ya namna ya kuboresha zaidi utekelezaji wa shughuli hizo. Vilevile, Mkutano huu ni chachu ya kuvutia mitaji kupitia mijadala inayofanywa na wadau mbalimbali kuhusu fursa za uwekezaji zilizopo katika sekta ya madini na namna ya kutumia fursa hizo kwa manufaa ya pande zinazohusika.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Kama ulivyojionea, Mkutano huu wa mwaka 2023 uliambatana na maonesho ya vifaa vinavyotumika katika shughuli za madini, bidhaa mbalimbali za madini pamoja na teknolojia zinazotumika katika shughuli

za madini. Kama nilivyokwisha sema mkutano huu ni jukwaa muhimu sana ambalo hutoa fursa kwa washiriki kujionea technolojia mbalimbali za kisasa zilizopo katika shughuli za utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, na uongezaji thamani madini. Mkutano huu pia huwezesha washiriki kujua maeneo yenye fursa za kuwekeza na kutumia nafasi hiyo kufanya majadiliano ya kiuwekezaji wakati na baada ya mkutano huu.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Katika mkutano huu kumefanyika mijadala mbambali katika maeneo yafuatayo;- fursa za uwekezaji katika sekta ya madini Tanzania na Afrika; teknolojia na ubunifu katika uchimbaji na utafutaji bora wa madini; uchimbaji endelevu na matarajio ya baadaye katika sekta ya madini; ufadhili wa miradi, changamoto za taratibu za usimamizi na fursa nchini Tanzania na Afrika Mashariki; Madini Mkakati katika kuzalisha nishati safi; uchenjuaji na uendelezaji madini katika mnyororo mzima wa thamani; kujengea uwezo wasimamizi na kukuza vipaji katika kuendeleza sekta ya madini.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Katika majadiliano yote yaliyofanyika washiriki wametoa michango yao mbalimbali yenye lengo la kujifunza, kuhamasisha ubunifu na uwekezaji katika sekta ya madini. Kutokana na majadiliano hayo zipo hoja ambazo zinatakiwa kushughulikiwa na Serikali ili kuboresha mazingira ya uwekezaji hapa nchini. Mimi na wenzangu Wizarani tunaahidi kuzishughulikia hoja hizo kwa ukamilifu.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Naomba nitumie fursa hii pia kuwahakikishia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwa Serikali kupitia Wizara ya Madini itaendelea kushirikiana nao katika shughuli mbalimbali za sekta ya madini kwa

manufaa ya pande zote mbili. Aidha, katika juhudi za kuwezesha Sekta ya Madini kuwa na maendeleo endelevu kwa manufaa mapana ya uchumi wa nchi yetu, Wizara itaendelea kuboresha taarifa za kijiolojia ili kuwezesha wadau kupata taarifa muhimu zitakazowawezesha kufanya utafutaji wa kina wa madini kwa ajili ya uanzishwaji wa migodi.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Kwa mara nyingine tena, napenda kuwashukuru washiriki wote wa Mkutano huu na kuendelea kuwahamasisha kuunga mkono juhudi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuiendeleza Sekta ya Madini. Aidha, nawakaribisha wawekezaji wote ambao wameona fursa za uwekezaji na wanahitaji msaada wa Serikali ili kuanza kuwekeza katika mnyororo mzima wa undelezaji madini nchini. Uwekezaji huo ni pamoja na utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, uongezaji thamani madini na biashara ya madini. Milango ipo wazi muda wowote, mimi pamoja na wenzangu wizarani tupo tayari kuwasiliza na kuwapa ushirikiano ili kwa pamoja tuiendeleze sekta ya madini kwa maslahi ya pande zote mbili.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,*** *baada ya kusema hayo, kwa heshima kubwa napenda nikukaribishe uweze kuzungumza na hadhara hii kisha utufungie rasmi Mkutano wetu.*

**Mheshimiwa Rais karibu sana**

DRAFT